BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

<u>BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI</u>

<u>MKUTANO WA KUMI NA SITA</u>

<u>Kikao cha Kumi – Tarehe 25 Septemba, 2024</u>

Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

## I. <u>HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:</u>

<u>Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi:</u>

Ripoti ya Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati kwa mwaka 2023/2024.

<u>Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:</u>

Ripoti ya Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati kwa mwaka 2023/2024.

<u>Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati:</u>

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati kuhusu Ripoti ya Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi juu ya Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati kwa mwaka 2023/2024.

<u>Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati:</u>

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati kuhusu Ripoti ya Wizara ya Ujenzi,Mawasiliano na Uchukuzi juu ya Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati kwa mwaka 2023/2024.

## II. MASWALI:

### Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais:

144. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais:

Tathmini iko vipi juu ya ongezeko la watoto wanaozaliwa na virusi vya HIV.

### Ofisi ya Rais, Ikulu:

162. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Ikulu:

Je, Zanzibar ina mafungamano yepi na Wazanzibari wanaoishi Canada, Vietnam, Urusi, na Kajikistan.

### Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:

210. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:

Tathmini iko vipi juu ya suala zima la kuchelewa kusikilizwa kesi mbali mbali katika Mahakama zetu kwa sasa.

### Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:

36. MHESHIMIWA BAKAR HAMAD BAKAR (Jimbo la Wawi) – Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inachukua juhudi mbali mbali katika kuitangaza Zanzibar kwa lengo la kuwavutia wawekezaji wa nje kuja kuwekeza.

(a) Tokea mwaka 2020 hadi leo hii, ni kampuni ngapi za nje zimewekeza Zanzibar.

(b) Je, ni miradi ya aina gani ambayo imewekezwa.

(c) Je, ni kiasi gani cha fedha ambacho Serikali imepata kupitia uwekezaji huo.

**Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:**

16. MHESHIMIWA BAKAR HAMAD BAKAR (Jimbo la Wawi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

Serikali hununua na kumiliki mali mbali mbali kama vile gari, hata hivyo, kumekuwa na changamoto ya usimamizi wa mali hizo.

Je, ni mfumo upi unaotumiwa na Serikali kusimamia mali zake.

**Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:**

253. MHESHIMIWA DKT. MOHAMMED ALI SULEIMAN (Jimbo la Mtambwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Kwa mujibu wa Sheria ya Usafiri wa Bahari Zanzibar ya mwaka 2006, Mamlaka ya Usafiri Baharini Zanzibar Maritime Authority (ZMA), imepewa mamlaka ya kusajili meli za ndani na nje. Pamoja na mamlaka haya ya kisheria kumekuwa na sintofahamu juu ya huduma hii inayotolewa na ZMA.

(a) Je, ZMA inaendelea kusajili meli za ndani na nje na meli ngapi zimesajiliwa katika kipindi cha 2020 - 2024.

(b) Je, ni mapato ya kiasi gani yamekusanywa kwa huduma hii ya kusajili meli inayofanywa na ZMA.

(c) Je, ni kwa namna gani Serikali inawezesha meli zilizosajiliwa na ZMA kutoa fursa kwa mabaharia wenye asili ya Zanzibar kufanya kazi.

254. MHESHIMIWA DKT. MOHAMMED ALI SULEIMAN (Jimbo la Mtambwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Kumekuwa na changamoto kwa mabaharia wa Zanzibar wanaofanya kazi katika meli za nje na kupelekea kukosa haki zao ikiwa ni pamoja na mazingira magumu ya kazi, kunyanyaswa na kukosa stahiki zao.

(a) Je, kwa takwimu Zanzibar ina idadi ya mabaharia wangapi wanaofanya kazi katika meli za nje.

(b) Je, Serikali ina sera na kanuni zinazosimamia fani na ajira za ubaharia nchini kwa mabaharia wazawa.

(c) Je, ni kwa namna gani Serikali imekuwa ikiwasaidia mabaharia kutatua changamoto zao na upi mkakati wa Serikali wa muda mrefu wa kuwa na Chuo cha Ubaharia Zanzibar.

## Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

249. MHESHIMIWA DKT. MOHAMMED ALI SULEIMAN (Jimbo la Mtambwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

Kiwanja cha mpira wa miguu cha Kisiwani, kiwanja cha Piki na kiwanja cha Tandavili ni viwanja vya mpira vinavyopatikana katika maeneo ya jimbo la Mtambwe, shehia ya Kisiwani na shehia ya Piki ambavyo hutumiwa na vijana wetu kwa ajili ya mchezo wa mpira wa miguu. Tokea kuanza kwa mradi wa ujenzi wa barabara ya Wete - Chake, viwanja hivi vilitumiwa kama maeneo ya kuweka kifusi na kuvifanya kushindwa kutumika.

(a) Je, ni lini viwanja hivi vitarudishwa katika hali yake ya kawaida na kutumika kwa shughuli za michezo.

(b) Je, ni yepi makubaliano ya Mkandarasi na Serikali juu ya kuvirudisha viwanja hivi katika hali yake ya kawaida.

250. MHESHIMIWA DKT. MOHAMMED ALI SULEIMAN (Jimbo la Mtambwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

Je, ni upi mkakati wa Serikali wa kujenga kiwanja chenye hadhi ya kucheza ligi katika ukanda kwa Kaskazini Pemba.

## Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale:

280. MHESHIMIWA DKT. MOHAMMED ALI SULEIMAN (Jimbo la Mtambwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale:

Inasemekana kwamba baadhi ya visiwa vilivyopo jimbo la Mtambwe vina historia kubwa, ikiwa ni pamoja na makaburi ya zamani kama vile makaburi ya Wareno yaliyopo katika kisiwa cha Mtambwe Mkuu, makaburi ya Wachina yaliyopo katika kisiwa cha Mahujuu (Kivumoni) na makaburi ya Waingereza yaliyopo katika kisiwa cha Funzi.

(a) Je, Serikali imewahi kufanya tafiti yoyote ili kuthibitisha ukweli wa historia hii na umuhimu wa maeneo haya ya kihistoria.

(b) Je, ni mkakati gani wa Serikali uliowekwa ili kuhifadhi na kutangaza maeneo haya ya kihistoria kwa ajili ya kuendeleza utalii wetu.

(c) Je, ni upi mkakati wa Serikali wa kuyatambua maeneo yote yenye historia katika nchi yetu na namna ya kuyahifadhi.

**Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi:**

79. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makaazi:

Nampongeza sana Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa uamuzi wake wa kuzikarabati nyumba za makaazi ya watu wa Michenzani.

(a) Ni lini ukarabati wa nyumba hizi utakamilika.

(b) Je, kuna changamoto yoyote inayopelekea zoezi la ukarabati wa nyumba hizi kutokwenda kwa kasi inayosubiriwa kwa hamu kubwa na wakaazi wa nyumba hizi zilizoasisiwa na jemedari na kiongozi shupavu wa Mapinduzi ya kumkomboa mwananchi wa Zanzibar.

**Wizara ya Afya:**

90. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Kwa kiasi gani maamuzi na malengo ya Serikali ya kuweka mkataba wa kutoa huduma katika sekta ya afya unaleta matokeo chanya.

93. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Saratani ni moja kati ya magonjwa yenye gharama kubwa sana kuyatibu.

Kwa kiasi gani Serikali inasaidia kuwapatia unafuu wa gharama za matibabu wananchi walioathirika na maradhi haya.

**Wizara ya Maji, Nishati na Madini:**

41. MHESHIMIWA BAKAR HAMAD BAKAR (Jimbo la Wawi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini:

    Asilimia kubwa ya wananchi wa Zanzibar wanatumia gesi kwa ajili ya kupikia ingawa gharama yake ni kubwa.

    Je, Serikali ina mkakati gani wa kupunguza gharama ya gesi ili kuongeza idadi ya wananchi wanaotumia nishati hiyo safi na salama kwa afya zao.

## III. HOJA ZA SERIKALI:

**Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi:**

Ripoti ya Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati kwa mwaka 2023/2024.

**Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:**

Ripoti ya Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati kwa mwaka 2023/2024.

**Zanzibar,**
**25 Septemba, 2024.**

**(Raya Issa Msellem)**
**KATIBU WA BARAZA.**